**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

***Email:* mpugusotc@moe.go.tz**
**mpugusotc@gmail.com**
***Unapojibu tafadhali taja:***
***Simu: 0733651948***

Chuo Cha Ualimu Mpuguso,
S.L.P 104,
**TUKUYU.**

***Kumb.Na. CCUM/U/4/VOL.3/76***

**Tarehe: 22.06.2026**

Ndugu:...................................................................................................................

**S.L.P...................................................................................................................**

**Kuh: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI 2026/2027**

**1.0 UTANGULIZI:**

Ninayo furaha kukuarifu rasmi kuwa, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuchagua kujiunga na Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya S*tashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi Mchepuo wa Sayansi ya Jamii kwa Lugha ya Kiswahili/Kiingereza katika Chuo cha Ualimu Mpuguso*. **Muda wa mafunzo ni miaka miwili (2). Kwa wanachuo wa Mafunzo ya Ualimu kwa njia ya masafa muda wa mafunzo ni miaka 3 hadi 4.** Baada ya kuhitimu mafunzo haya, mhitimu atakwenda kwenye *Mafunzo ya Uanagenzi* (Interniship) kwa mwaka mmoja kwa kuzingatia miongozo ya serikali. (**Walimu Kazini hawatahusika na Uanagenzi**).

**2.0 MAHALI CHUO KILIPO**

Chuo cha Ualimu Mpuguso kipo Mkoa wa Mbeya, Wilaya ya Rungwe. Kipo kilometa 10 kutoka kituo kikuu cha mabasi cha Tukuyu. Ukitokea Mbeya panda mabasi ya Kyela na shuka kituo cha mabasi cha Ushirika, Kadhalika anayetoka Kyela atashuka kituo cha mabasi Ushirika. Kutoka Ushirika panda bodaboda nauli ni kati ya **Tsh.1000/= hadi 2,000/=** (Chuo kipo umbali wa kilomita 3 kutoka kituo cha mabasi cha Ushirika).

**3.0 KURIPOTI CHUONI**

Unatakiwa kuripoti chuoni tarehe **17/08/2026**, utahitajika kuhudhuria mafunzo kabilishi (Orientation Course) yatakayoanza mara moja. Ukichelewa kwa majuma mawili tangu tarehe ya kuripoti chuoni hutapokelewa na nafasi hiyo atapewa mtu mwingine. Mara baada ya kuwasili chuoni fika ofisi ya Usajili kusajiliwa. (***N.B.Wanachuo wa Elimu ya Ualimu kwa Masafa watapewa taarifa kuhusu kituo na tarehe ya kuanza mafunzo kabilishi***).

**Ili usajiliwe unatakiwa uwe na vitu vifuatavyo:**

3.1 Barua *ya kuitwa kujiunga na Chuo (i.e.Barua hii ya maelekezo ya kujiunga na Chuo).*

*3.2 Cheti* halisi cha kumaliza kidato cha Nne/Sita (Certificate of Secondary Education Examination /Advanced Certificate of Secondary School Examination) pamoja na ‘School Leaving Certificate-Original

3.3 Cheti halisi cha kuhitimu Mafunzo ya Ualimu Daraja IIIA (Grade A Teachers Certificate Examination -GATCE) au Result Slip kwa wale waliomaliza kidato cha sita/Ualimu mwaka 2026.

3.4 Cheti halisi cha kuzaliwa- (Original Birth Certificate).

3.5 Walimu kazini, pamoja na maagizo ya hapo juu (3.1-3) wanapaswa kuja na ***barua ya ruhusa ya kwenda masomoni*** **kutoka kwa mwajiri wake**.

3.6 **Pamoja nakuja na vyeti** halisi ni lazima uje na nakala (fotokopi) za vyeti vyote kwa ajili ya kuweka kwenye faili la kumbukumbu binafsi. **Mwanachuo atakayekuja na nakala za vyeti bila vyeti halisi hatapokelewa.**

3.7 Cheti cha daktari/medical examination form**, ijazwe na daktari wa Hospitali ya Serikali ya Wilaya.**

3.8 Picha 2 za rangi (passport size).

**4. 0 VIFAA**

4.1 Mashuka mawili rangi bluu bahari (light blue) yasiyofumwa, blanketi 1, mto 1, foronya 2 bluu bahari zisizofumwa, neti ya kujikinga na mbu, ndoo ya lita 10 na taulo.

4.2 Vyombo vya chakula, sahani 1, kikombe 1, bakuli 1, kijiko 1, galoni ya lita tano ya plastiki kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa yaliyochemshwa.

4.3 **Nguo za michezo**: track suti ya bluu bahari 1, raba jozi1na bukta 1 rangi ya bluu bahari (**Wanachuo kwa njia ya masafa haiwahusu**).

4.4 Daftari zisizopungua 12 (counter book (Quire2au3), kalamu za wino na risasi, mkebe wa Hisabati.

4.5 Karatasi rimu 1 (A4) rangi nyeupe yenye karatasi 500 kwa kila mwaka wa masomo.

4.6 Vitabu mbalimbali vya kozi ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa masomo ya mchepuo wako.

4.7 Mihutasari miwili ya shule ya msingi kwa masomo yako ya mchepuo.

4.8 **Vifaa halisi vya Elimu ya Kujitegemea:** *Wanachuo wote waje na jembe lenye mpini na panga.(**Wanachuo wa Ualimu kwa njia ya masafa hawatahusika na agizo hili**).*

4.9 Kishikwambi, Simu Janja, Kompyuta mpakato inayoweza kuunganishwa na mtandao wa intaneti (**Kwa Wanachuo wa stashahada kwa njia ya masafa**).

**5.0 ADA YA CHUO**

Ada ya mafunzo ni **Tsh 450,000/=** kwa mwaka kwa wanachuo wote, Ada hii inaweza kulipwa yote au kwa awamu mbili **Tsh. 225,000/=** kwa kila muhula. Ada italipwa kwa mtandao (GEPG) baada ya kutengenezewa namba ya malipo (Control Number) na Mhasibu wa Chuo pindi ufikapo chuoni **AU** fanya mawasiliano na **Mhasibu wa Chuo** namba **0756353737 au Msajili** namba **0756976608** ili kupata namba ya Malipo ya Ada. ***Muhimu*****: USILIPE FEDHA YA ADA KWENYE AKAUNTI YA MICHANGO.**

**6.0 FEDHA YA MICHANGO KWA MAHITAJI MBALIMBALI**

Utatakiwa kulipa jumla ya **Tshs 210,400/=** kwa ajili ya Michango mbalimbali ya chuo, kama ilivyo changanuliwa kwenye jedwali hapo chini.

| Na. | Michango | Kiasi (Tshs) | Maoni |
|---|---|---|---|
| 1 | Serikali Ya Wanachuo | 5,000/= | Kwa Mwaka |
| 2 | Fedha Ya Huduma Ya Kwanza | 10,000/= | Kwa Mwaka |
| 3 | Usafi Na Mazingira | 20,000/= | Kwa Mwaka |
| 4 | Godoro Hutolewa Hapahapa Chuoni | 10,000/= | Kwa Mwaka. Usije Na Godoro. |
| 5 | Usajili Na Kitambulisho | 20,000/= | Inalipwa mara moja ukiwa Mwaka wa Kwanza. |
| 6 | Michezo | 30,000/ /= | Kwa Mwaka |
| 7 | Ulinzi | 30,000/= | Kwa Mwaka |
| 8 | Ukarabati | 25,000/= | Kwa Mwaka |
| 9 | Bima ya Afya | 50,400/= | Kwa Mwaka (Wasiyo na Bima ya Afya ya Taifa) |
| 10 | Mahafali ya Chuo | 10,000/= | Kila Mwaka |
| **JUMLA KUU** | | **210,400/=** | |

**7.0 ADA NA MICHANGO KWA WANACHUO WA STASHAHADA YA UALIMU KWA NJIA YA MASAFA**

| **Na.** | **Michango** | **Kiasi** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|
| 1 | Huduma ya kwanza (Matibabu) | 10,000.00 | Kwa mwaka |
| 2 | Usajili na Kitambulisho | 20,000.00 | Inalipwa mara moja mwaka wa kwanza |
| 3 | Serikali ya Wanachuo | 5,000.00 | Kwa mwaka |
| 4 | Ukarabati | 25,000.00 | Kwa mwaka |
| 5 | Elimu ya Michezo | 30,000.00 | Kwa mwaka |
| 6 | Usafi na Utunzaji wa Mazingira | 20,000.00 | Kwa mwaka |
| 7 | Ufuatiliaji na uendeshaji wa mafunzo | 40,000.00 | Kwa mwaka |
| | **Jumla ya Kuu** | **150,000.00** | |

**N.B** Malipo yote ya fedha ya michango yaingizwe kwenye Akaunti ya Chuo Cha Ualimu Mpuguso, Namba **61401000012 NMB** jina la akaunti ni **MPUGUSO TEACHERS' COLLEGE GENERAL ACCOUNT**. Lipia kwenye tawi lolote la **NMB** lililo karibu nawe uje na **BANK PAY SLIP**. Usije na fedha Taslimu ya **michango** chuoni.

**8.0 SARE YA CHUO**

8.1 Vazi rasmi ni **Suti nyeusi jozi moja** na **Bluu nyeusi** (dark bluu) jozi moja. (Suruali **nyeusi** na **Bluu nyeusi** (darkblue) zenye upindo (turn up) na ***upana wa suruali chini uwe inchi 17,*** mkanda wa ngozi mweusi na soksi nyeusi (Wanaume), sketi **nyeusi** na **Bluu nyeusi,** soksi nyeupe (Wanawake) mashono ya sketi yasiwe na marinda (shona solo) ***izidi inchi 5 kutoka kwenye magoti.***

8.2 Mashati ya mikono mirefu, rangi ya bluu bahari (light blue) jozi mbili(2) yanapatikana chuoni kwa **Tsh 15,000/=** kwa shati moja.

8.3 Koti **jeusi** na **Bluu nyeusi** rangi ya suruali/sketi pamoja na Tai rangi nyeusi na **Bluu nyeusi**.


8.4 Usinunue nguo (sare) za mtumba **hakikisha sare (suti) imeshonwa vizuri na fundi.**

8.5 **T-Shirt** yenye nembo ya chuo inapatikana chuoni kwa **Tsh. 15,000**.00 .

8.6. Viatu vya ngozi rangi nyeusi vya kamba (viwe vya kufunika na visigino vifupi) .

8.7 Wanachuo wa kike wa Kiislamu wanatakiwa kuvaa hijabu ya bluu bahari (**light blue)** urefu usawa wa kifua**.**

**NB**. Kwa mashono ya sare angalia ilivyo katika michoro namba 1 na namba 2 ifuatayo:




**9.0 MAAGIZO MUHIMU KWA AJILI YA AFYA NA MAHAFALI YA WANACHUO**

9.1. Mwanachuo anashauriwa aje na fedha kwa ajili ya matumizi binafsi.

9.2 **Kwa mwenye kadi ya bima ya afya anashauriwa aje nayo.**

**10.0 CHAKULA**

Chuo hutoa chakula aina ya ugali (sembe), wali, kande, uji, chai, mkate, maharage, nyama, matunda na mboga za majani. **Chuo hakitoi chakula maalum (Special diet) kwa wenye matatizo ya kiafya**.

**NB. Mwanachuo ambaye hatakamilisha mahitaji yaliyoorodheshwa hapo juu hatapokelewa Chuoni**.

**11.0 SHERIA NA KANUNI ZA MWENENDO BORA WA MWANACHUO**

Katika kipindi chote cha mafunzo mwanachuo atatakiwa kutii sheria za Nchi na Kanuni za Mwenendo Bora wa Mwanachuo atakazopewa na chuo.

**12.0 MWISHO**

Jumuiya ya Chuo Cha Ualimu Mpuguso inakutakia maandalizi mema ya safari ya kuja chuoni.

**KARIBU SANA**




STEPHEN J. MGIMBA
**MKUU WA CHUO**
**Mobile: 0683 155 290**

**NAKALA**: Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali, Eneo la Mtumba,
S L P 10,
**40479 DODOMA.**

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,
Wilaya ya Rungwe,
S.L.P. 34,
**TUKUYU.**

Mthibiti Ubora Mkuu wa Shule (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe,
S. L. P.148,
**TUKUYU.**

Afisa Elimu (M),
S.L.P 754,
**MBEYA.**

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Chuo,
S. L. P 104,
**TUKUYU.**

## GOVERNMENT OF TANZANIA
## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**PART A:**

TO: The Medical Officer

From: Mpuguso
Teachers' College.

..............................................

..............................................

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teachers course.

A: 1. (a) Eye – sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Venereal Diseases
(e) Leprosy
(f) Limbs
(g) Epilepsy
2. Neuroses
3. Other serious diseases.

B: Blood Group

Date : ..........................

Signature..............................
Official Stamp

*************************************************************************

**PART B:** **MEDICAL CERTIFICATE.**

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named student that he/she is physically fit/unfit and mentally *fit/unfit for a full time teacher Education course.

- (a) Eye – sight............................................................
  (b) Hearing..............................................................
  (c ) Limbs...............................................................
  (d) Speech..............................................................
  (e) Leprosy.............................................................

II. Neuroses.........................................................................

III. Other serious diseases.....................................................

IV. pregnancy.......................................................................

**Date:..............................................Signature...............................**
**Official Stamp**